




Namba ya Mshiriki katika Utafiti. []-[]-[]

[Jinsi ya kujiunga kwenye tovuti ya mtandao]

- Namba ya mshiriki katika utafiti inaingizwa kiotomatiki kwenye tovuti wakati mshiriki anachanganua msimbo wa QR na simu janja. (Ili kufanya hivyo, ni lazima simu hiyo iwe na kamera na programu ya Daum au NAVER.)
- Tafuta sensa ya watu na makazi katika ukurasa wa taarifa za tovuti. Bofya na kisha uweke namba ya mshiriki katika utafiti.
- Andika hapo census.go.kr kwenye upau wa anwani. Kivinjari kitakupeleka kwenye tovuti ya utafiti na hapa itakuwa ni lazima uweke namba ya mshiriki katika utafiti.

 <p>Simu janja (Kichanganuzi cha QR)</p>	<p>1. Changanua msimbo wa QR kwenye ukurasa wa habari</p>	<p>2. Ingia (Namba ya mshiriki katika utafiti huwekwa kiotomatiki)</p>	<p>3. Kujithibitisha na kuweka nenosiri</p>
 <p>Simu janja (tovuti)</p>	<p>1. Jiunganishe kwenye tovuti ya sensa ya watu na makazi</p>	<p>3. Andika hapo namba ya mshiriki katika utafiti</p>	<p>4. Kujithibitisha na kuweka nenosiri</p>
 <p>Skrini ya kompyuta</p>	<p>1. Jiunganishe kwenye tovuti ya sensa ya watu na makazi 2. Bofya "Shiriki katika Utafiti wa Mtandao"</p>	<p>3. Namba ya mshiriki katika utafiti</p>	<p>4. Kujithibitisha na kuweka nenosiri</p>

Maadhimisho ya Miaka 100 ya Sensa ya Watu

Sensa ya 2025

Sensa ya Pili ya Watu na Makazi

Utafiti wa mtandao na simu: 2023.10.16~10.31

Utafiti wa kutembelea nyumba ambazo hazikujibu: 2023.11.1~11.17

※Kwa maelezo zaidi, tafadhali nenda kwenye tovuti ya sensa ya watu na makazi

(www.census.go.kr)

Sensa ya Watu na Makazi ni takwimu muhimu iliyo dhinishwa kitaifa na pia hutumiwa kama data ya marejeleo ya kutambua na kutathmini sera za kitaifa, utafiti wa kitaaluma na usimamizi katika sekta ya kibinafsi. KOSTAT inafanya utafiti wa majaribio ili kutambua maeneo ya uboreshaji na kujiandaa vyema kwa ajili ya Sensa ya Watu na Makazi ya 2025.

Utafiti mahiri usio wa ana kwa ana utafanywa kati ya tarehe 16 Oktoba (Jumatatu) na 31 Oktoba (Jumane) na washiriki wataweza kukamilisha utafiti kupitia kompyuta/simu janja (census.go.kr au msimbo wa QR) au kituo cha kupiga simu (bila malipo kwa nambari 080-000-2025, kuanzia saa 3 Asubuhi hadi saa 1 jioni). Watu ambao watakamilisha utafiti katika kipindi cha utafiti mahiri (16 Oktoba hadi 31 Oktoba) watapata nafasi ya kujishindia zawadi ndogo kupitia droo ya bahati nasibu.

Nyumba ambazo hazijibu utafiti kupitia Mtandao au simu zitatembelewa (wakati wowote kati ya Jumatano tarehe 1 Novemba na Ijumaa tarehe 17 Novemba) na wafanyakazi wa KOSTAT ambao watafanya mahojiano ya ana kwa ana katika nyumba za watakaojibu.

Kulingana na Kifungu cha Sheria cha 33 na 34 kuhusu Takwimu, maelezo utakayotoa yatalindwa kikamilifu ili yasitumike kwa madhumuni mengine isipokuwa kuandaa matokeo ya utafiti. Kwa hivyo, tunaomba ushirikiano wako kamili katika kukamilisha utafiti huu.

Nyumba yako imechaguliwa kuwa ndio itajibu katika utafiti wa majaribio wa 2 wa Sensa ya Watu na Makazi ya 2025.

Tafadhali soma upande wa nyuma wa mwongozo huu kwa maelekezo ya kina kuhusu jinsi ya kushiriki katika utafiti.

Mabadiliko ya kesho huanza kutokana na utakavyosimulia.

Statistics Korea